

**(ii)Miraba miwili sambamba**
Katika mfumo huu, miraba miwili huwekwa pamoja na nafasi kati jozi moja ya mraba na nyingine ni mita 3.0 hadi 4. Katika mfumo huu nafasi kati ya mche mmoja na mwingine ni mita 0.70 -1.0.

Kwa kawaida upandaji hufanywa kwa mfumo wa zigzag kwa miche kati ya mraba mmoja na mwingine kupishana kwa umbali wa nusu ya umbali kati ya mche wa mraba mmoja na mwingine.



**5.5.2 Muda wa Kupanda**
Mkonge upandwe wiki moja au mbili kabla ya msimu wa mvua kuanza.

**6.0 UTUNZAJI WA MKONGE**
**6.1 Udhibiti wa magugu**
Udhibiti wa magugu ufanywe kwa kutumia majembe ya mkono na viuagugu kama Tomcil, Multiglyphosate, Roud up, Karachi na nyinginezo kadri ya maelekezo ya wataalam wa kilimo wa eneo husika. Njia nyingine ni kwa kutumia mimea jamii ya kunde sentro, yogoyogo, fiwi na Glycine javanica.



**6.2 Virutubisho vya udongo**
Mmea wa Mkonge kama ilivyo mimea mingine unahitaji madini mengi kutoka ardhini ili ukue vizuri na usipate magonjwa. Madini muhimu ni pamoja na Potasiamu (K), Fosforasi (P), Chokaa (Ca) na Naitrojeni (N). Virutubisho hivyo vinaweza kupatikana kwa kuweka mbolea za mimea na wanyama au za viwanadani kama CAN, UREA, TSP, NPK , MOP na nyingezo.

**7.0 UVUNAJI WA MKONGE**
Kwa kawaida uvunaji wa Mkonge hufanywa baada ya miaka mitatu kwa majani yaliyokomaa Majani yanayotakiwa kuvunwa ni lazima yasipungue urefu wa sentimeta 60. Na ambayo kwa kawaida ndiyo yanakuwa tayari yamekomaa vizuri.Jani lile lililo katika mwinuko usiozidi nyuzi 450 ndio linalotakiwa kuvunwa. Majani ya yavunwe kwa kutumia kisu kikali na yavunwe kwa kukata kwenye eneo ambalo jani linaungana na shina.

**8.0 USINDIKAJI WA MKONGE**
Mkonge uliovunwa unatakiwa kusindikwa ndani ya masaa 48 ili kupata singa (nyuzi) zilizo bora. Mashine za kusindikia mkonge zipo za aina tatu ambazo ni kubwa, za kati na ndogo kabisa. Ndogo kabisa hutumiwa na wakulima wadogo, za kati hutumiwa na wakulima wa kati na kubwa hutumiwa na wakulima wakubwa (estate)

**9.0 Matumizi ya Mkonge**
Mkonge hutumika kutengeneza kamba, magunia, mazuria, vikapu na urembo. Mkonge pia hutumika kwenye ujenzi, magari, kutengeneza dawa, kuzalisha gesi ya kupikia, kuotesha uyoga na mabaki ya mkonge baada ya kuchakata hutumika kurutubisha udongo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**
**BODI YA MKONGE TANZANIA**


# KILIMO CHA MKONGE



## 1. Zao la Mkonge
Mkongeni zao la muda mrefu la kibiashara ambalo huvunwa majani na kusindikwa ili kupata nyuzi. (Singa)

## 2. Maeneo yanayofaa kwa kilimo cha mkonge
Mkonge unatakiwa kupandwa kwenye maeneo yenye sifa zifuatazo;

**Udongo**
Udongo unaofaa kwa kilimo cha mkonge ni ule wenye rutuba ya kutosha na usiotuamisha maji. Ardhi inayofaa kwa kilimo cha Mkonge ni lazima iwe na udongo wenye kipimo cha tindikali (pH) kati ya 7.0 – 7.5

**Mvua**
Mkonge unahitaji mvua kati ya milimita 625-1,250 kwa mwaka.

**Mwinuko**
Mkonge unastawi vizuri kwenye mwinuko wa kati ya mita 100-1,800 toka usawa wa bahari.

**Joto**
Mkonge unahitaji hali ya hewa ya joto la sentigredi 25 - 33 (25-33$^{0}$C). Mkonge unahitaji vipindi virefu vya jua ili kuwa na singa nyingi na nzito. Hivyo, mkonge hautakiwi kupandwa kwenye kivuli.

## 3. Aina za Mkonge
Kuna aina nyingi za mkonge nchini Tanzania, ila kuna aina kuu mbili zinazolimwa kwaajili ya biashara ya singa (nyuzi) ambazo ni;-

### 3.1 Agave sisalana
Ni aina ya Mkonge asilia uliyoingizwa kwa mara ya kwanza nchini na Dr.Hindorf kutoka Yucatan

### 3.2 Mkonge Chotara (Hybrid 11648)
Aina hii ni matokeo ya mchanganyiko wa kisayansi (cross breeding) ya Agave Angustifolia na Agave Amaniensis

## 4. Mbegu za mkonge
Kuna vyanzo viwili vya mbegu za mkonge vinazovyotumika kwa sasa kama ifuatavyo:

### 4.1 Machipukizi/maotea
Baada ya kupanda mkonge shambani, machipukizi huota kutoka kwenye mkonge uliopandwa.



*Picha ikionesha maotea yaliyochimbwa kwa kuzingatia ubora*

### 4.2 Mbegu za Kitalu/Vikonjo
Mbegu za kitalu ni vikonyo vinavyopatikana kwenye mlingoti wa Mkonge uliozeeka ambapo uchambuliwa vizuri, hupandikizwa na kutunzwa kwa ufasaha.



*Mbegiu zinazoandaliwa kwenye kitalu*

## 5.0 UPANDAJI WA MKONGE SHAMBANI
### 5.1 Matayarisho ya shamba
Utayarishaji wa shamba la Mkonge ufanyike kabla ya msimu wa mvua kuanza kwa kukata na kuchoma vichaka, kung'oa visiki, kuondoa/kuchoma visiki vilivyong'olewa, kulima kwa kina cha sentimeta 30-45 na kulainisha udongo.

### 5.2 Uchaguzi na upangaji wa miche
Miche ya kupanda iwe bora na inashauriwa iwe na urefu wa sentimeta 50 – 70 na uzito wa kilo 2 – 4. Aidha, miche ipangwe katika madaraja kulingana na ukubwa wake.

### 5.3 Uchimbaji wa miche
Kwa kawaida jembe la mkono au sululu hutumika kuchimbia mbegu. Ni muhimu kuwa mwangalifu shina lisikatwe au kujeruhiwa ili kuzuia hatari ya kushambuliwa na wadudu pamoja na magonjwa ya kuoza kwa mmea.

### 5.4 Utayarishaji wa miche kabla ya kupanda
Baada ya miche kuchimbwa, mizizi ikatwe kwa uangalifu bila kuharibu shina (bole) na majani yaliyonyauka yaondolewa. Ikiwa yanatumika maotea inashauriwa miche ikusanywe kutoka kwenye shamba lenye Mkonge usiozidi miezi 36 na wenye afya. Urefu wa miche ya maotea uwe ni kati ya sentimita 40 -70.

### 5.5 UPANDAJI WA MKONGE
#### 5.5.1 Mifumo ya Upandaji
Kuna mifumo miwili ya upandaji Mkonge inayotumika ambayo ni:

**(i)Mfumo wa Mraba mmoja**
Mfumo wa Mraba mmoja ambapo nafasi kati mraba mmoja na mwingine ni mita 3.0 hadi 4 na nafasi kati ya mche mmoja na mwingine ni mita 0.70 -1.0.